TANGAZO LA SERIKALI Na. 60 la tarehe 31/1/2025

SHERIA YA AJIRA NA MAHUSIANO KAZINI,
(SURA YA 366)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 98(2)(p))*

KANUNI ZA ADA ZA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI ZA MWAKA 2025

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ada za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi za Mwaka 2025.

Tafsiri

**2**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Ada" maana yake ni malipo kwenda kwa Tume kwa ajili ya kupata huduma zilizoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi; na

Sura ya 300

"Tume" maana yake ni Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Taasisi za Kazi.

Ada za Tume

**3**. Ada zilizoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi zitalipwa kwa Tume kulingana na huduma zilizoainishwa kwenye Jedwali hilo.

Msamaha wa kutokulipa ada

**4**.-(1) Serikali haitawajibika kulipa ada kuhusiana na shauri lolote itakalofungua au litakalofunguliwa dhidi yake mbele ya Tume.

(2) Endapo mkataba wowote ulioingiwa na Jamhuri ya Muungano na nchi nyingine yoyote unaeleza kwamba ada hazitalipwa kwa ajili ya shauri lolote, ada zilizoainishwa katika Jedwali hazitalipwa kuhusiana na shauri husika.

Sura ya 21

(2) Mtu ambaye amepewa msaada wa kisheria chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria kuhusiana na shauri aliloanzisha au lililoanzishwa dhidi yake hatalipa ada anazopaswa kulipa kwa Tume chini ya Kanuni hizi.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza, iwapo

atajiridhisha kwamba kuna mazingira maalum yanayomzuia mtu kulipa ada anayopaswa kulipa chini ya Kanuni hizi, kutoa msamaha kwa mtu huyo kutolipa ada husika.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 3)*

ADA ZA HUDUMA ZA TUME

| NA. | HUDUMA INAYOTOLEWA | KIASI CHA ADA KWA KILA HUDUMA |
|---|---|---|
| 1. | Kusajili Fomu CMA F.1 | 10,000/= |
| 2. | Kusajili Fomu CMA F.1B | 10,000/= |
| 3. | Kuomba nakala ya mwenendo iliyothibitishwa (kwa kila ukurasa) | 100/= |
| 4. | Kupata nakala ya ziada ya tuzo au uamuzi mdogo (kwa kila ukurasa) | 200/= |
| 5. | Kusajili hati ya Makubaliano | 20,000/= |
| 6. | Kuwasilisha nyaraka nyingine yoyote ambayo haijabainishwa katika Jedwali hili | 2,000/= |
| 7. | Majibu ya maombi mengine yoyote | 2,000/= |
| 8. | Maombi ya kupitia jalada la shauri | 5,000/= |
| 9. | Kuwasilisha maombi chini ya Hati ya dharura | 100,000/= |
| 10. | Maombi ya kuongeza muda wa kusajili nyaraka nje ya muda | 20,000/= |
| 11. | Kusajili shauri la madai ya gharama | 30,000/= |
| 12. | Kuwasilisha Taarifa ya Pingamizi na Kiapo Kinzani | 20,000/= |
| 13. | Kurekebisha Nyaraka za Maombi | 10,000/= |
| 14. | Maombi mengine yoyote | 10,000/= |
| 15. | Maombi ya kuchelewa kusajili mgogoro | 10,000/= |
| 16. | Maombi ya kutengua uamuzi wa upande mmoja | 20,000/= |
| 17. | Maombi ya kurejesha mgogoro | 20,000/= |
| 18. | Maombi ya kibali cha kukubaliwa kutoa huduma za msingi wakati wa mgomo au kufungia nje | 200,000/= |
| 19. | Maombi ya kutambua huduma kama huduma muhimu mbele ya Kamati ya Huduma Muhimu | 300,000/= |
| 20. | Kusajili mgogoro mbele ya Kamati ya Huduma Muhimu | 300,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 21. | Ombi la kuteuliwa kwa huduma ya chini zaidi mbele ya Kamati ya Huduma Muhimu | 300,000/= |
| 22. | Maombi ya kuhamisha shauri | 20,000/= |
| 23. | Kusajili mgogoro wa haki za kiasasi | 100,000/= |
| 24. | Kusajili mgogoro wa kupunguza wafanyakazi | 100,000/= |
| 25. | Kusuluhisha mgogoro ambao haujawasilishwa rasmi mbele ya Tume | 100,000/= |

Dodoma,
21 Januari, 2025

RIDHIWANI J. KIKWETE
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*